Com. Bishop Njoroge: Sawa. Haya kwenda kwa nyingine.

Daniel Weloto: Ikiwa mtu ameshikwa na kitu kama exhibit, kitu kama bangi labda mtu ajawai ona na kweli atashikwa na unaona askari anatembea na bangi, anakupeleka kortini anashtakiwa kweli amepatikana nayo na mwenye ajawahi ona. Askari akishika mtu, lazima kuwe na mtu mwingine hapo ili awe shaidi ndio apelekwe kortini. Mtu akishtakiwa kwa haraka, mara unaenda kortini “advocate ako Nakuru”, “advocate ako Kisumu”, siku zinahirishwa. Tuwe na committee ya wazee wale ambao wanaweza kusaidia korti. Asante sitaendelea na mengi kwa sababu nitapeana memorandum.

Com. Bishop Njoroge: Asante. Umesema hutaki mtu akiua mtu na unajua ameua hutaki advocate?

Daniel Weloto: Advocate hapana.

Com. Bishop Njoroge: Kuja kumtetea?

Daniel Weloto: Hata na yeye awe killed.

Wakoli: *Lisina liase bananga bali Wakoli.*

Translator: My name is Wakoli

Wakoli: *Nono ese ndoma ndi,*

Translator: What I want to say,

Wakoli: *Onyala waba ne bakeni,*

Translator: You can have visitors.

Wakoli: *Wekhale mungo ne masalao.*

Translator: You have sat in the home with your mother in law,

Wakoli: *Ne basikari becha mungo.*

Translator: Then the police come to your home.

Wakoli: *Ne babona mwekhale, si bareba sichilila ta.*

Translator: They just see you sitted but they don't know what is going on,

Wakoli: *Ne obona babukula omulosi okhusalila omukhasi!*

Translator: You see them arresting your mother in law!

Wakoli: *Ne bakhuboa kimikoye ne masalao.*

Translator: They arrest you alongside your mother in law

Wakoli: *Se bariakho ta.*

Traslator: They don't fear.

Wakoli: *Ne babukula masalao chana bamufwala kamalwa.*

Translator: They put beer on your mother in law

Wakoli: *Wakhekana oli kamalwa se kabelekho ano tawe ibele echai,*

Translator: Even if you say there was no beer, they will say--

Wakoli: *Ne bakhaya oli kamalwa.*

Translator: They will say it was beer.

Wakoli: *Ne barakho masalao oyo enjaka.*

Translator: They put bang on your mother in law.

Wakoli: *Nono efwe sekhuli ne buuru ta.*

Translator: We have no freedom,

Wakoli: *Kenya selikho ne buuru ta.*

Translator: Kenya has no freedom.

Wakoli: *Basikari bali ne buuru.*

Translator: The police are the ones with freedom.

Wakoli: *President wefwe niye ali ne buuru.*

Translator: The President is the one with freedom.

Wakoli: *Akhukhalakila busa ali siosi siosi kha mukhole.*

Translator: He can decide for you what to do.

Wakoli: *Nono efwe, khukhola khurie?*

Translator: What do we do?

Wakoli: *Khakhube busa khurio.*

Translator: Let us just be like that.

Wakoli: *Nono ese kakase kawa.*

Translator: Mine is finished.

Com. Lethome: Bado hujamaliza. Unataka nini kuhusu askari akienda kushika mtu, unataka ashike namna gani?

Translator: Wenya basikari bakhole barie?

Wakoli: *Basikari ne becha, barebe bali ko, ali mungo muno mukhola si?*

Translator: The police should come quietly and ask what is going on.

Wakoli: *Namwe barebe bali omusasi we mungo muno ali wae?*

Translator: or even ask the head for the family.

Wakoli: *Mala ese nje mbole ndi mungo muno, kamakosa se kalikhomo ta.*

Translator: Then I explain if there is nothing wrong in the home.

Wakoli: *Bukhupani bulimo? Ne ese mombolela ndi bukhupani bubeleo.*

Translator: If there is any fighting, I will say that ...

Wakoli: *Ne bosu bamanye. Nembalangile,*

Translator: If I have called them

Wakoli: *Nono senabalangile ta, becha si?*

Translator: Now that I have not called them, why should they come?

Com. Lethome: *Orio Musakhulu.*

Wakoli: *Kalaa musakhulu.*

Com. Bishop Njoroge: Asante sana. Karibu.

Vitalis Wamalwa: Naitwa Vitalis Wamalwa. Ningependa kuongea matatu hivi. Jambo la kwanza, ni wasted knowledge. Wasted knowledge, pengine ningependa kuguzia ya kwamba kuna watu wengi wakubwa wamesoma kabisa, wako skilled in various fields, lakini kwa sababu ya hii mambo ya retirement, wanaenda retirement na sisi tunaendelea kusumbuka. Tena, kulingana na hayo maneno, unaona ni mtoto wa shangazi, au wa nyanya analetwa pale. Ningependekeza kwamba, hawa watu wamesoma sana, hata kama miaka yao imeisha na wame-retire wameenda nyumbani, wangukuwa kwa advising committees wawe wakiwa consulted everytime, wakija kuona maneno yako namna gani. Kwa mfano, sijui kama itawezekana- lakini kama mzee akienda nyumbani, ni vizuri aje ashauri watu---

Interjection. Com. Bishop Njoroge: -----(inaudible)

Vitalis Wamalwa: Pointi nyingine ni kwa upande wa miwa. Hasa sisi wakulima tungependa tujue utaratibu wa miwa. Kwa mfano, miwa inapokatwa kutoka shambani, ikibebwa kilometer fulani unalipa kiasi fulani. Ikifika weigh bridge wakipima tones fulani, hujui wanalipa pesa ngapi. Kutoka hapo inapoingia ndani, vitu vyote vinakatwa tujue kama ni stake wamekuletea, stake moja ya kupanda ina-cost pesa ngapi- ili, mkulima awe ukijua umebeba stake ngapi unajua ulikatwa pesa kiasi fulani kwa sababu hapa Nzoia, miwa inaenda huko na wanakuambia walikupa stake tano na kumbe walikupa stake moja ya kupanda. Sasa tunataka waki-supply hiyo seed, we sign somewhere, tujue tuli-receive hii, tukienda huko tunajitetea. Kwa sababu hata unaweza shikanisha wewe na jirani yako ako huko, wanasema “enda uchukuwe huko mbegu”. Wanamwaga mara tatu watu wanaenda usiku wanabeba lakini wanaku-charge. Sasa hiyo tunaona ni hasara.

Way of worship: mimi ningependa serikali pia kama wameruhusu kila mtu ashiriki kwa kanisa lake anapenda, lakini pia Serikali ingeteua kamati wafuate njia vile watu wanaomba. Sisi tunaona wakubwa wetu haswa, wamejenga makanisa especially ile inaitwa Free Masons, inaingiwa makubwa makubwa kama makubwa kama haya yamesimama hapa. Tunasikia wanaenda kwa mgongo- na hao ni wakubwa. Sasa tunashindwa watasema namna gani. Wakati ule unaenda kusema huko, unawekwa ndani ya gari kwa boot. Utashtukia uko kwa nyumba yenye hakuna mlango. Sasa tunaomba serikali ichunguze vile watu wanaenda kuomba, wafuate utaratibu. Kwa mfano, tuseme mimi ni Mkatoliki, waende waone hawa watu wanaeneza neno la Mungu au wanaeneza maneno ya shetani.

Com. Bishop Njoroge: Tumepata hiyo.

Vitalis Wamalwa: La mwisho, ningependa kuona- sijui serikali itatumia mbinu gani- mwenzagu ameguzia maneno ya askari. Kwa sababu, mambo ya TTK wamesema yamekwisha lakini ukienda kama gari imejaa. Tungependa utaratibu uwe kama wa Uganda. Kama Nissan tunajua inachukua watu kumi na wawili na inaenda, tungependa ichukue watu exactly. Sijui wata-effect namna gani kwa sababu bado haya mambo ya kujaza kwa barabara yako na accidents bado zinatokea lakini kwa sababu utakuwa na kijisanduku cha kiberiti uweke kitu ndani utupe chini mzee achukue, wewe utaenda lakini accident itakuwa mbele. Asante.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much.

Fred Nyongesa: Kwa majina naitwa Fred Nyongesa Torofu. Yangu ningependekeza juu ya upande wa Kenya police- mimi nasikia kwa matangazo kila mara wanatangaza kuwa sisi tuko huru na police sasa ndiye mkubwa- hata mkubwa kwa President!

Ukikutana na askari badala ya kukuuliza unaenda wapi, anakuharakisha, kofi ndio hiyo, amekushika na kukuchukua, mtafika huko- pengine distance kama ile choo iko huko, ndio ajue wewe haukuwa na makosa. Kwa hivyo, mimi nalia askari warekebishe kidogo. Police walikuwa tu wa kulinda wakubwa sio kuharakisha wakubwa ingawaje, mimi si mkubwa. Lakini hata nilikuwa na mkubwa akaharakishwa, hata tai ikamnyonga bila yeye makosa kuwa na mokosa yoyote. Kwa hivyo, harassment ya police irekebishwe.

La pili, ningetaka kuzungumzia maneno ya baba na mama nyumbani. Bibi na bwana nyumbani- kuna sheria kutoka tangu zamani. Kuna Mukasa, kuna Sub-chief mpaka kuna Chief. Wakipigana kwa boma Chief na Mukasa ndio huwa wanamaliza.

Com. Lethome: Unajua kuna tofauti baina ya kupigana na kupiga. Nasikia hawa Wabukusu wanaita *khusola*. Sasa hiyo *khusola* sio kupigana, ni vita. Pande moja ndio inapiga ingine. Hiyo utasema ichukuliwe hatua gani? Unajua kuna tofauti mimi na wewe tukipigana na kuna tofauti wakati unapiga mtu ambaye hakupigi- anapiga tu mayowe.

Com. Bishop Njoroge: Na pia unaona siku hizi watu wanapiga hata wanaua. Sio kama zamani wazee hata kama anapiga anajua bado ni mke wake. Siku hizi sio wazee wa zamani. Wazee wa zamani hawakuua au kuumiza. Kwa hivyo lazima tuweke sheria.

Fred Nyongesa: If you put that law, then the wife are going to beat them.

Com. Bishop Njoroge: Sheria ya domestic violence ikiwekwa ni party zote mbili. Bibi hawezi kupigwa na bwana hawezi kupigwa na labda, itawasaidia kuzungumza kwa sababu, hakuna kitu kizuri kama mazungumzo. Hata kukiwa na shida gani, inatengenezwa na nini? Na mazungumzo.

Com. Lethome: Lakini wewe toa maoni yako vile unataka.

Fred Nyongesa: Maoni yangu, hiyo sheria itoe kwa sababu sisi wanaume ndio tunapigwa- hapa hapa tu. Ukikosana na yeye, anakimbia huko na police nao wakiona bibi, hawawezi kuongea na wewe, ni kupigwa tu. Sasa hiyo sheria itolewe ibaki kwa sub-chief na Chief na Mukasa kama zamani.

Ya tatu, ninalilia juu ya representative kama mimi mkulima wa Nzoia sugar company. Mimi ni mkulima niko na miwa na

Kanduyi hapa, MP yule ambaye tunachagua, huyu akija anasema ‘mimi ndiye nitaweza nikimbie hata office ya President mpaka waje walipe wakulima’. Lakini tukishapitisha yeye, anaenda anakaa Nairobi. Hashughuliki hata ukihesabu hapa MPs au Minister, tangu tuchague miaka mitano vile imekwisha, hakuna minister ameingia hapo. Kwa hivyo MPs, wale tunachagua-wale representative wote wa kusaidia washughulike na maneno yetu hapa kwa vile sisi ndio tumewaandika. Waje washughulike na sisi hapa kwa shida ile tuko nayo. Sio kusimama kwa miti na kusema ati kwa President hatuwezi fika. Wewe ulisema unafika, tena ni kitu gani kiimekuzuia wewe kufika kwa President?

Com. Bishop Njoroge: Sawa. Point nyingine.

Fred Nyongesa: Imekwisha.

Com. Bishop Njoroge: Imekwisha?

Fred Nyongesa: Mh.

Com. Bishop Njoroge: Kuja ujiandikishe hapa.

Patrick Kitui: Kwa majina naitwa Patrick Kitui. Ningependa kuongea juu ya recruitment of Police, Army na Navy. Tuna watu wengi huwa wanaenda interview lakini wakati unafika huko, ukiangalia ukikagua vitu vyenye wako navyo, unaona wana faili. Halafu wakija unasikia wanasema wengine wamechukuliwa kitambo eti list imekuja na watu wako kwa kiwanja. Kwa nini wasichukue hao, na list hii ilitokea wapi? Sasa, tunataka tuwe na fair system of recruitment. Kwa mfano hivi sasa ukiuliza mtu kama anataka aende police, atakwambia kuwa kama angekuwa Eldoret angeenda haraka lakini, sehemu kama za Bungoma unajua unajua-- hatutaki hiyo. Tunataka kama mzaliwa wa Bungoma kama unajisikia kwenda kwa wanajeshi, unajisikia huru kwenda huko. Sio eti utaenda namna gani? Kwa mfano, watu wengi wana-qualify lakini, kama hawachukuliwi, tunaona majambazi. Kwa maoni yangu naona hawa watu wenye wanastahili wafanye hiyo kazi na wakikataliwa, hasa hawakui na alternative kwa maana wanajiona wako vizuri, sasa wanaamua wapambane na hao watu wamechukuliwa na serikali. Ndio munaona majambazi ndio hawa, wanavamia police kwa maana waliwakataa na wanataka wawaonyeshe kuwa pia nao wako na ujuzi.

Com. Bishop Njoroge: Thank you very much. Kuja ujiandikishe hapa.

Ann Adhiambo: Kwa majina naitwa Adhiambo, mimi ni mkaaji wa Nzoia na ningependa kuzungumzia juu ya elimu- bursary funds. Mimi kwa upande wangu ninaweza kusema hivi; education is a basic need for all Kenyans irrespective of gender and ethnic ground. Since the government’s duty is the need to eradicate poverty, hunger and provide education among Kenyan society, I feel little has been done concerning the education sector. Alliance boys high school and Starehe Boys Centres were

established for the less fortunate and bright children from poor families. Now, it happens to be for the well to do families in our midst. The bursary was meant for students from poor families so as to pursue their education especially in secondary schools. But right now, the bursary funds are for pupils from the politically connected families and no wonder most of them are pupils of men and women sitting in the Board of Governors. My proposal is that, this bursary fund should be placed under an independent department in the Ministry of education or Social services so as to cater for education of pupils from poor families or those of HIV/Aids parents, so that they can get education as the others.

Secondly is about traditional liquor: kama kuna maswali mtaniuliza baadaye. As well as we can appreciate the banning of traditional liquor by the government, I do feel that the banning was orchestrated by the colonial governors who felt that their security would be at risk if the black Kenyans were left free to brew their beer. This law is not African- oriented and I can say by example; our neighbouring country like Uganda and Tanzania, they have practiced it and it has proved more successful. I do feel that, the government should uplift that law so as the menace of police officers who are empowered to arrest and prosecute those found in the offence should stop that corruption of soliciting money from the culprit. That will also help the government to fight this cause of corruption. My proposal is that, the government should legalize traditional liquor this being busaa, mnazi and chang'aa so as to easy congestion in our prison. I say and I mean, this should not be legalized freely but there must be a law to govern this business and set the time limit for those who want to consume, it may be from 2.00 pm to midnight so that employees cannot be affected.

Sasa, wazee mtusaidie tafadhali kwa sababu, kuna wazazi wetu ambao wamefiwa na baba zetu- yaani wajane. Hawana namna yeyote na kama hawezi kuuza hii chang'aa especially wakati huu kuna ugonjwa wa ukimwi, hakuna haja mama mzee wa miaka arobaini au hamsini, apewe shilingi hamsini kwa ajili ya ugonjwa wa ukimwi ati anaenda kujisaidia. Kama hii pombe kweli, mtuwachie na muunde mtusaidie. Hatuchagui watu kwenda kukaa huku juu kufunga tai lakini tunawachagua watusaidie. Hii pombe iwekwe, vile vile Uganda na Tanzania. Kwa kusema ukweli, hata Uganda huwezi kupata mlevi- mtu mwenye ameenda Uganda na Tanzania, kweli kuna mlevi unaweza kutana naye njiani? Kwa vile hatuna freedom ya kutosha, mtu ananunua chang'aa ishirini "anapiga touch" ili police asimpate na police akimpata, anataka pesa kutoka kwake na tena anamwaachilia. Sasa kama police kama anaweza kupata pesa kutoka kwa yule mtu, mpeane percentage fulani na pombe iwepo.

Kitu cha pili, kuna hivi vitu vya freedom from hunger walk. Hata subchief yuko hapa, tunapewa forms za kujisaidia wale watu hawajiwezi upande wa chakula na unapata, hata huyo Mukasa ndiye anapata mahindi mingi kuliko yule mtu mwenye alitakikana apate hayo mahindi. Sasa hapo pia mtusaidie. Na mimi vile ninaongea hivi; hata mimi ninaye mtoto na nilipata nje ya ndoa na ninataka nijisaidie na ninataka niepuke na maneno ya ukimwi haya- ambapo sina kazi lakini nimesoma. Kwa hivyo ninaweza sema niuze chang'aa ili nipate mapato yangu na mtoto wangu pia, lakini Police wamekuwa wagumu. Nikishikwa wanachukua pesa kwangu. Sasa kuchukua pesa na kupeana percentage fulani, nilipe gani mzuri? Tunataka mtusaidie, kama pombe iwepo, iwepo na kama haiwezi kuwepo na hata police asipate hongo kutoka kwangu. Ni hayo tu.

Com. Lethome: Hebu ngoja kidogo. Unajua mwaka uliopita sijui kama ulisoma kwenye vyombo vya habari. Kuna watu walikufa, wengine wakupoteza macho mpaka leo hii ni vipofu na watu wengi wamepoteza maisha kwa sababu ya hii pombe haramu. Hata busaa imeumiza watu wengine- lakini una uhuru wa kutoa maoni yako. Sasa how do you take care of that now?

Ann Adhiambo: Mimi najua vizuri sana. Hata wakati huu, Nzoia kuna pombe inaitwa miti ni dawa na ninajua hiyo pombe, hakuna tofauti ya miti ni dawa na busaa. Kwa sababu hii pombe inatengenezwa na mwanadamu vile hata busaa inatengenezwa na mwanadamu. Sasa kama kutakuwa na vitu kama hivyo na pombe iweko, bora isiwe kumi kumi ya kuumiza watu. Unajua kuna watu wanatafuta pesa na kuna watu wanataka pesa, kuna haki yao. Sasa hao wenye wali-introduce mambo ya kumi kumi ya kuuu watu- na hata sijawahi sikia hata mmoja alishikwa hata kama siko karibu na Nairobi, lakini siwezi kujua kama hawa watu walichukuliwa hatua. Sasa kama kutakuwa na vitu kama hivyo- pombe hiyo imekuwa tangu kitambo lakini sasa pombe hata kupimwa, tunaweza kubali ipimwe bora iwe pombe nzuri na iwe na permit, watu wakunywe na wawe salama. Kuliko mtu apige chang'aa ya ishirini na aende afe. Mwenye amemuuzia anashtakiwa, na yeye amepoteza maisha yake.

Kitu cha tatu ni kwamba, kama mtu amuuawa mahali fulani, tafadhali police itusaidie kuchukulia hawa watu hatua. Hakuna haja mtu ameuawa, familia yake inasikia uchungu na police wanakula hongo ya shilling elfu tano na mtu amepoteza maisha yake. Tusaidiane. Serikali ilikuja kulinda usalama wa watu wa Kenya na itusaidie. Mambo ya hongo tuache. Hata barabarani ajali nyingi zinatokana kwa mambo ya hongo. Mtu anapewa shilling ishirini na watu wanapoteza maisha ya watu ishirini. Hiyo tafadhali pia mtusaidie. Lakini upande ya pombe nitarudia; kama hiyo pombe mtatuachilia huru na ipimwe pia wajue kama ni pombe nzuri watu wanaweza kunywa au ni pombe inawezadhuru watu.

Com. Bishop Njoroge: Hebu mama nikuulize swali?

Ann Adhiambo: Niulize baba niko hapa kujibu maswali.

Com. Bishop Njoroge: Hawa watu wanakunywa chang'aa ya ishirini na wanakufa, wanauwawa na nini?

Ann Adhiambo: Anakunywa pombe akiwa na njaa- hajakula, lakini anaona afadhali akunywe chang'aa na hii chang'aa hana freedom. Anakunywa haraka haraka ili police wasimpate. Na katika ile hali, anakunywa chang'aa, "anapiga touch" na anajua police anakuja---

Intejction: Com. Lethome: Tumia language ambayo tunaweza kukuelewa.

Ann Adhiambo: Language gani unataka nitumie?

Com. Lethome: Unamaanisha nini ukisema "anapiga touch?"

Ann Adhiambo: Yaani, anakunywa haraka- katika ile harakati asikutwe na mtu. Unajua mwizi akikuibia kitu chako, si anakua na wasiwasi. Mara anakimbia nini. Sasa ndio hiyo ninasema “touch.”

Com. Bishop Njoroge: Chang’aa haitaji mtu ---

Ann Adhiambo: Chang’aa haitaji mtu apige touch. Kama watu wengi ni walevi sana wanaamkia pombe na unajua hawali kitu. Ni chang’aa tu. Sasa hii chang’aa akiipata anajua “mimi nikikutwa na askari, nitatoa elfu moja”. Sasa kitu kilichoko, nipige touch na niende.

Com. Bishop Njoroge: Akinywa pole pole hatashikwa?

Ann Adhiambo: Akinywa pole pole watamshika apelekwe police.

Com. Bishop Njoroge: Lakini kama akinywa pole pole atakufa?

Ann Adhiambo: Hawezi kufa. Wewe uko na freedom, wewe unaenda hoteli umenunua chakula chako, unakula haraka aje kama mwizi? Si unakula pole pole Sasa hiyo, ndiyo tunataka yaani akunywe pole pole na ajue tu kuwa hivi vitu vimewekwa uhuru, tunalipa percentage fulani. Iwe consumer, iwe na nani bora tu iwe na percentage fulani. Lakini hii ya touch, anakufa kwa sababu amepiga touch na matumbo yake iko bure, hakuna kitu amekula na inamuua. Mwenye ameza anapelekwa ndani. Na hata hivyo akipelekwa ndani, hakuna hatua anachukuliwa.

Com. Lethome: Unasema nini kuhusu vita vya nyumbani, mama kupigwa na baba kama discipline, unasemaje?

Ann Adhiambo: Mama kupigwa na baba, hata hivi vitu vilikuwako kitambo na siku hizi vimeisha ambapo siku hizi kukutana na mama anapigana na baba- mtu kama mimi mamangu hawezi pigana na baba kwa sababu mimi ni mkubwa. Kama kuna ugomvi wa nyumba, baba na mama watakaa chini na waongee. Na ikiwa kutakwa na kitu kama hicho- najua kuna watu bado wanafanya hivyo vitu- ni Chief, Sub-chief na Mukasa. Hawa wanafaa waongee hayo maneno, ikiwazidi ndiposa wapeleke mbele lakini si ati mtu amepigana na bibi yake na police wanaenda kumchukua, Police wako hapo kuchunga usalama si kuchunga vile watu wamegombana. Kuna watu wanaweza kuwa wana-renew mapenzi na police wanaingilia namna gani. Lazima kwa nyumba wapigane lakini si police waingilie. Ndio maana kuna Chief na Subchief na Mukasa.

Com. Bishop Njoroge: Unakaa hapa, unafanya kazi gani?

Ann Adhiambo: Mimi, vile unanion hivi, mimi ni casual wa Nzoia sugar company katika department ya agriculture na mimi

kazi yangu yenye ninafanya, mimi napanda miti. Nafanya afforestation na kibarua yangu inakuwa for three months and after three months, wana-renew. Hata kweli, mzee umeongea vizuri. Mimi nimekaa hapa, nilikuja 1998 as a volley baller. Nimefanya hii kazi, nacheza mpira, nafanya kibarua. Hata confirmation peke yake sijawai pewa. Pia hiyo mtusaidie. Kama mimi hivi sasa ni mtu mkubwa, nimefanya vibarua vya miezi tatu na nimeshindwa. Hata saa hii imefika mpaka lazima utoe hongo ndio hicho kibarua yenye unatakikana upate. Sasa nitafanyaje kama mimi single mother nitafanyaje? Ukimwi ndio hiyo imejileta, iko mlango.

Kitambo, unajua mzee, Ukimwi ilikuwa inaua mtu na watu walikuwa hawajagundua. Ukimwi ilikuwa kwamba, mtu anakupa 50,000 na anakuambia- after amekupa ukimiwi anakuwambia 10,000 itakuwa ya sanduku. Wakati huu, Ukimwi unapewa bure, na tusaidiane. Ukimwi wakati huu Uganda hakuna. Kama kweli mnaweza kujua tu dawa zinawezapatikana za kusaidia watu, kuna watu wengine hawajiwezi lakini wana huo ugonjwa. Sasa tafadhali mtusaidie. Wazazi wetu kama hao au hata mimi, mnisaidie nisiwe na mawazo nyingi ili ukimwi naye isinipeleke haraka. Mnaweza kunisaidia na mawaidha fulani kwa sababu watu wengi wenye wanapata ukimwi ni wale hawajiwezi.

Mambo ya squatters: mnasema kuna watu squatters na kuna watu wenye mashamba hekari thelathini, arobaini na hawayalimi. Kwa nini kweli hatuwezi toa hii jina squatter na tugawie hao watu wengine hata walime pia. Mashamba yanakaa bure na wanasema hili ni shamba la mtu fulani na hilo shamba ni mfano kwake, na wengine wanaitwa squatter, squatter inakuja aje? Mtu kama ana shamba kama hekari 10 au 20 na hana uwezo wa kulima na wenye wanakaa squatter wanakaa squatter wana nguvu walime hayo mashamba. Halafu yeye, aende aongee na serikali. Kwa sababu shamba haiwezi kukaa bila kulimwa na kuna wenye wanaitwa squatter, hayo maneno pia hatutaki. Tunazungumzia kwa hayo mtusaidie.

Com. Lethome: Haya asante Ann, tumeshukuru sana.

Ann Adhiambo: Asante.

Com. Lethome: Nafikiri huyu ndiye alikuwa mtu wa mwisho. Njoo ujiandikishe Ann. Ala mbona tumekaa tumemaliza watu. Ann ndiye alikuwa mtu wa mwisho? Nani mwingine anataka kuzungumza? Basi dakika moja moja. Tulikuwa tumemaliza bwana. Haya endelea. Sema majina.

Hezbon Nitia: Kwa majina naitwa Hezbon Nitia na ningependa kupendekeza yafuatayo: jambo la kwanza ni recruitment ya forces. It should be done at the divisional level and not district kwa sababu, unaweza kupata district iko na vijana karibu elfu hamsini wanataka kuchukua vijana kumi peke yao. Hapo kuna corruption kwa sababu mwenye anajiweza ndio ataenda. Sasa kama impelekwa division itakuwa rahisi kwa sababu watu watakuwa wachache sana.

Jambo la pili, most industries zinatakikana ziwe privatized kwa sababu, if an expatriate can come from outside na anakuja hapa

Kenya, yeye hajui Mkikuyu, hajui Mluhya, hajui Mjalu anajua a qualified person. Kama wewe umequalify utaandikwa kazi. Lakini kampuni zikiwa kwa sisi wenyewe, watu wengi hawatapata kazi kwa sababu mtu fulani hajiwezi hata kama ni expert. For example, kama Kicomi huko Kisumu ilianguka kwa sababu watu wa hapo wenyewe walitaka kujiandika wenyewe na hawangeweza ku-produce according to their labour.

Jambo lingine ni mambo ya MPs au mambo ya Parliament. Either a President or an MP before are declared to be fit to stand somewhere, he has to declare his wealth. Inatakikana asimame mahali na wengine ambao wote wanataka kuwa MPs, they also have declare their wealth. Baada ya hiyo, government should not sponsor any person who is doing campaign. Mtu atumie wealth yake mwenyewe kutafuta hicho kiti na ajue anaenda kusaidia watu. Na mambo ya hongo kwa kupata kura isikuweko. Kuwe na watu kutoka nje wa kusimamia kura- wasiwe watu hapa wenyewe kwa sababu wa hapa wenyewe huwa wanaharibu kura. For example, like a Kikuyu will be in Bungoma, kura ya Councillor inaharibika, kura ya President kumbe anapigia mtu wa kwao.

Jambo lingine ni kuhusu pesa. Pesa ya Kenya isiwe na sura ya mtu yeyote. Iwe na court of arms badala ya kuweka sura ya mtu kwa vile tunaona after five years, President anatoka, hatutaweka kila miaka tano kichwa cha President mwingine kwa pesa. Pesa iwe na court of arms badala ya kuwa na sura ya mtu. Ni hayo tu.

Com. Lethome: Asante.

Joram Wanjala: Kwa jina langu naitwa Joram Wanjala na ningependa kusema kuwawa serikali inalia ya kwamba uchumi umezoroteka- na kuna sehemu ambayo ningeweza kuzungumzia ya kwamba, hasa wenye tunaishi kwa bara bara hii, unaona ya kwamba serikali inapoteza a lot of tax kwa sababu ya mambo ya corruption. Unaona kama, labda vitu vinatoka Uganda vinakuja Kenya. Wakati mwingine unaona gari moja ikienda weigh bridge, mdosi ako mbele na amebeba vitu ambavyo si halali, analakiwa mbele anapewa pesa na hao wanakuja wanapita tu. Akifika kama labda Webuye hapa, anarusha kitu anawaambia “ndio hao wanakuja nyuma”, wanapita tu. Kwa hivyo pesa nyingi tunapoteza ambayo ingekuwa kama tax kwa sababu pesa ambayo ingekuwa kwa serikali inarudi kwa police.

Mimi naona, wa-increase pesa ya askari ndio wafanye kazi nzuri kuliko sasa wenyewe kuharibu uchumi wa nchi yetu ya Kenya. Vitu vinatoka nga'mbo ambavyo vinahitaji tutoe pesa lakini kwa sababu askari wanataka wakulie humo, wanaachilia vinapita na serikali inapoteza pesa na tunajua uchumi umezoroteka. Point ya pili ni kwamba, suspect asiteswe. Anateswa mpaka anakufia kwa jela na yeye hana makosa. Mwishowe, wanathibitisha ya kwamba huyu mtu hana makosa, na amepigwa anaenda kukufia nyumbani. Sasa mtu yeyote unless witness akuweko, asipelekwe speed kiwango ya kuumizwa kabla hajaweza kuthibitisha kwamba ana makoa. Sasa hilo jambo, ninaona kwamba watu wengi wanaumia sana, na hali hiyo inafanya watu wanapoteza masha yao. Ni hayo tu, asante sana.

Com. Lethome: Dakika mbili umalize, tutamaliza na huyo mzee ambaye alikuwa ameziandikisha, akaenda kazini kidogo.

Johnstone Wabwire: *Khu masina bananga bali Johnstone Wabwire.*

Translator: I am called Johnstone Wabwire.

Johnstone Wabwire: *Ndakachulakho khu lubeka lwa balanganga bali dictatorship khu biongozi.*

Translator: I am talking about dictatorship in our leadership.

Johnstone Wabwire: *mbara ra nandi mungo khubechanga nende oimelela singa papa.*

Translator: In the home we have a father,

Johnstone Wabwire: *Ne mala ne khufananisha khurio nende sibala, aba ali President.*

Translator: when we give that analogy he is like the President.

Johnstone Wabwire: *Papa mungo ali olindile email ye banyelee.*

Translator: The father looks after the welfare of those he is in charge of.

Johnstone Wabwire: *Nga President na lindile email ye wananchi.*

Translator: Just like the President looks after the welfare of the country

Johnstone Wabwire: *Nono omundu nomuele, nomuwelesia enafasi ye khukhulindila email yowo,*

Translator: If you have entrusted someone to look after your wealth,

Johnstone Wabwire: *Sanyala kacha mumusilu katibia chikhafu, mala oendelee khuba ne naye ta.*

Translator: He cannot go with the cattle and loose them in the forest and then you continue keeping him.

Com. Lethome: Come to the point.

Johnstone Wabwire: *Epoint yange niyo ino,*

Translator: This is my point,

Johnstone Wabwire: *Omwami nga omwimilesi we sibala President,*

Translator: like now the President,

Johnstone Wabwire: *Sali ao khubukula kamatoka, Lundi apange kumusiru uri khukhwama ao khucha khuola aao.*

Translator: He should not have a fleet of vehicles,

Johnstone Wabwire: *Khusuta basikari,*

Translator: To carry Police, Ministers,

Johnstone Wabwire: *Ba delegates, kho bacha khukhola e-conference mala eli sisindu sili binafsi tawe.*

Translator: To do a conference which is an individual's ...

Johnstone Wabwire: *Bibiene ebyo bibindu bilala bilareranga enjala musibala, mala birera corruption.*

Translator: That is what is bringing down the country, bringing hunger and corruption.

Johnstone Wabwire: *Alubeka wa corruption,*

Translator: About corruption,

Johnstone Wabwire: *Khuli nende barumikhi banyelele balanga bali basikari;*

Translator: We have people or our servants called police;

Johnstone Wabwire: *Khu ministry ya defense,*

Translator: In the ministry of defense,

Johnstone Wabwire: *Babandu bano babaweesia chisilingi chingali sana.*

Translator: They have been given a lot of money.

Johnstone Wabwire: *Kenya babapungusie, mala bekolasi ekho khulondekhana nende sibala nge ne si, babandu nga bali musibala siosi.*

Translator: They should reduce their salary to match with the other civil servants.

Johnstone Wabwire: *Mala busikini se bulabakho ta.*

Translator: Then there will be no poverty.

Johnstone Wabwire: *Ndikhi nja busa kwa ufupi, sikila mulomile basi chisaa chinditi nicho.*

Translator: I am rushing because I am told that there is no time.

Johnstone Wabwire: Bursary fund:

Translator: Bursary fund:

Wabwire: Chisilingi nichyo batenganga khuyeta bandu bali banyala be...bakesi, mala khukhwama mu-family chikhanyala ta,

Translator: Bursary is meant for the bright and poor children.

Com. Lethome: Can he recommend?

Johnstone Wabwire: Lakini nono abundu anao abechanga oli chisilingi chirura khu-Serikali, chiicha khuolela abandu bano,

Translator: But when it come to giving out the bursary,

Johnstone Wabwire: Se chola chya yeta abandu ba bakesi mu-family chioli poor tawe.

Translator: It is hardly directed to the poor.

Com. Lethome: What do you want yourself?

Johnstone Wabwire: Nono ese ndolelele khusaye mbu khubira khumukanda kwa Constitution Review Commission,

Translator: I am recommending to the Constitution Review Commission that,

Wabwire: Babukule bandu khukhwama muchi-areas bamanyile bandu masikini bano, mala banya basuna bachia ebweni bayeta chi-family chyabwe.

Translator: Let there be a committee from the locals who know those children so that they can recommend their rights.

Johnstone Wabwire: *Baane chisilingi to the right people.*

Translator: So that it is given to the right people.

Johnstone Wabwire: *Khu county council,*

Translator: About county council,

Johnstone Wabwire: *Babusia chisilingi khukhwama khu raia.*

Translator: They collect money from citizens,

Johnstone Wabwire: *lakini se balikho ne buyeti bwosi bwosi khubafanyi biashara tawe.*

Translator: They don't offer any services.

Johnstone Wabwire: *Nono kenyakha bawekesie bafanyi biashara bano chisilingi nga chi-loan,*

Translator: They should give the business people loans,

Johnstone Wabwire: *bapanue bibiashara biabwe,*

Translator: To expand their business.

Johnstone Wabwire: *mala babukulekho profit ne baila nga khurunga chi-license.*

Translator: So that they can take a bit of profit to pay for the licenses.

Johnstone Wabwire: *Eshida ye chikasi mu Kenya selabakho tawe.*

Translator: There will be no problem of employment in Kenya.

Johnstone Wabwire: *Khulapungusia bujambazi musibala.*

Translator: We shall reduce thuggery in Kenya.

Johnstone Wabwire: *... besie khubasikari.*

Translator: About defense on police,

Johnstone Wabwire: *Basikari, musibala syefwe sino, babawesia bunyali bwakhila.*

Translator: Our police are given too much power.

Johnstone Wabwire: *Onyola omukhasi akhalomana ne papa mungo,*

Translator: Even when a wife is quarreling with the husband.

Johnstone Wabwire: *Omusikari anyala kawesia mama enafasi khukona ewewe.*

Translator: The mother will be given an opportunity to go and share a place with the policeman.

Johnstone Wabwire: *Mala ne bamayo, solalomalomakho liosi liosi tawe.*

Translator: Then a man will have nothing to say.

Johnstone Wabwire: *Nekhali, obirirra busa musikhupo ... khwicha khukhuboa direct.*

Translator: Then you will just go for imprisonment.

Johnstone Wabwire: *Nono abwene aobele ndasabanga Serikali mbo,*

Translator: I am requesting the government

Johnstone Wabwire: *Batase muda ya khutreina basikari ne bali mukambi.*

Translator: Policemen should be retrained for a longer time.

Johnstone Wabwire: *Ne mu-area mwosi khubechenge nende youth khubirira khu basasi,*

Translator: So that, in an area we should have youth through parents.

Johnstone Wabwire: *Khuchagua bandu banyala batatua chishida chye muching , khubeela khuli nende chikholo tofauti tofauti.*

Translator: So that, we can now form our local committee plus clansmen to kind of solve domestic problems.

Johnstone Wabwire: *Banyala bakhuyeta khumala eshida khulondekhana nende sikhale.*

Translator: to resolve those domestic problems traditionally,

Johnstone Wabwire: *Khulondekhana nende e-community mu-area muno.*

Translator: according to the community in that area.

Johnstone Wabwire: *Shairng of powers.*

Translator: Sharing of powers.

Johnstone Wabwire: *Ese ndolesia nandi sibala sia Kenya,*

Translator: I say that Kenya,

Johnstone Wabwire: *Sili sibala silimo chi-district zaidi ya hamsini.*

Translator: has more than 50 districts.

Johnstone Wabwire: *Lakini onyola mbo buongosi bwalola lubeka lulala luong'ene.*

Translator: it seems it is partial administration.

Johnstone Wabwire: *Haya, khuli ne chi Province munane.*

Translator: We have eight provinces.

Johnstone Wabwire: *Mundu anyala kama ariena mu-Province ndala, aruka kumwaka kuno, Lundi kukwicha luno aruka, kukwicha luno aruka?*

Translator: So how can they dominantly have one person from each province---

Com. Lethome: What do you recommend?

Johnstone Wabwire: *Sio ndikomenda mbo, kenyebwa babukule bubwami bakaba buli chi-district, chi-Provinces, Khukhwama khu Province mpaka khu District.*

Translator: there should be distribution of leadership in provinces.

Johnstone Wabwire: *Ndikho ngachula khu njala,*

Translator: I am talking about hunger

Johnstone Wabwire: *Sibala siefwe sia Kenya silikho ne njala tawe.*

Translator: We should not have hunger in Kenya

Johnstone Wabwire: *Sibala siefwe sili ise bulimi.*

Translator: this is an agricultural country.

Johnstone Wabwire: *mala ne sikhaya nono Serikali khubela mbo seli nende chi-powers chingali khuyeta balimi ta,*

Translator: Because the government does not support the farmers,

Johnstone Wabwire: *khunyola mbo mavuno kaba matiti, kaba asi,*

Translator: We see the harvest is less.

Johnstone Wabwire: *Nono khwenya bapungusie egarama ye bulimi,*

Translator: They should reduce expenses in farming,

Johnstone Wabwire: *mala omulimi na nyolile mavuno kewe*

Translator: so that the when the farmer gets his harvest,

Johnstone Wabwire: *kalayeta khurusia enjala musibala.*

Translator: it will reduce hunger.

Johnstone Wabwire: *kali kario.*

Com. Lethome: Thank you. Haya mtu wa mwisho kabisa.

Charles Masika Musungu: Naitwa Charles Masika Musungu, na hapa Nzoia niko kikazi, na nyumbani ni Mihanga, mahali panaitwa Matiku, Busia District. Nina mambo matatu. Mimi mwenyewe sijaelimika, lakini nitaongea mambo matatu.

Kitu cha kwanza, mwenzangu ameguzia na ilikuwa ndani ya roho yangu. Kwa sababu nilikuwa hapa, nikawa namba thirty three. Sisi wengine kama wazazi, hatujiwwezi. Lakini unakuta ile bursary inakuja, itaenda kwa Assistant chief, tajiri mwenye yuko na wengine, na wengine- walimu- zinaenda huko. Lakini utakuta shuleni masikini kweli wa mwisho watoto wako nyumbani.

Com. Lethome: Unapendekeza nini?

Charles: Napendekeza hapo nikisema, Serikali ikitoa sheria ifuatilie sheria, Kwa sababu Serikali inasema lakini haifuati. Hiyo ndio shida inayoumiza maskini. Kitu cha pili, utawala. Maskini asiposoma, atatawaliwa miaka yote; kama vile wanihubiria katika Biblia, Waisraeli wakati walikuwa katika Misri, na Yosufu vile alikufa, wakaanza kusema ya kwamba, Waisraeli, wakiwa wanataka kuzaa, watoe watu wa kuenda kuwazalisha, na waue watoto wanaume ili “wasije tena wakatutawala”. Hiyo inamaanisha ya kwamba, uchumi usipofikia maskini, inaoneka maskini natawaliwa na ana watoto, na ataishi na ujinga milele.

Com. Lethome: Sasa unataka tufanyeje ndio maskini waache kutawaliwa?

Charles: Nataka, Serikali ikitoa bursary, au ikitoa maendeleo fulani, iangalie masikini naye abarikiwe. Ya tatu, namalizia-nimekuwa kwa radio mara kwa mara, maoni ya usiku, maoni... lakini wakati watu wanatoa ma-point za manufaa, unakuta mtu mwenye anaandika haandiki hizo point. Anaziwacha. Hiyo ndio shida inayoendelea katika Kenya. Kwa sababu, mtu unaweza kuongea point, na kweli hiyo point ukiangalia ni point, unakuta mtu kwa radio anasema hapana hiyo imekwisha, time imekwisha, wacha tu hivyo---

Com. Lethome: Sasa unapendekeza nini?

Charles: Naona hapo, sasa inaonekana kwamba Serikali kutuletea kutaka maoni, inaonekana kwamba wenyewe wameamua kitambo, na yale wanataka kwa raia, haina maana- wanataka kuwapumbaza.

Com. Lethome: Hebu wacha nikuambie kitu kimoja. Hapa uko uhuru kusema kile unachotaka. Don't beat about the bush. Come straight to the point. Unataka kusema nini? Usiogope chochote. Elewa sheria imesema, mwananchi wa Kenya ana uhuru kusema kile anachotaka. Ukitaka kuchambua Rais, chambua. Ukitaka kuchambua Commission, chambua, Kwa hivyo, don't beat about the bush. Come straight to the point.

Charles: Vile nazungumza, unashika vizuri. Nimesema ya kwamba nimekuwa katika radio, maoni ikiendelea, mtu aki-shoot point unakuta mtu mwenye anammoja anasema kwamba “saa imekwisha, saa imekwisha” haandiki hiyo. Sasa hiyo napendekeza ya kwamba, inaonekana ya kwamba, muna sheria yenu, lakini kutafuta kwa raia, hamuna haja kuandika ma-point hizo.

Com. Lethome: unajua hujapendekeza sasa. Unataka nini? *Wenya shi?*

Charles: Nataka Serikali iweke mkazo. Mtu akitoa neno, lifuatiwe na lichunguzwe. Ni hayo tu.

Com. Lethome: Sasa ndio imeingia kabisa. Orio musakhulu. Nafikiri sasa kwa hayo maoni moto moto kabisa, tumefikia mwisho wa kikao chetu kwa siku ya leo na watu wa Nzoia tunawashukuru sana. Tumepata maoni ambayo tangu tuje hapa

